**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Wizara ya Maliasili na Utalii Utalii

IDARA YA WANYAMAPORI
WILDLIFE DIVISION

# Mwongozo wa kutenga na kuendesha Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori nchini Tanzania

**Please note: All illustrations of the original have been removed in this electronic version. It is therefore not identical with the original.**

IDARA YA WANYAMAPORI

# Mwongozo wa kutenga na kuendesha Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori

---

Barabara ya Nyerere, Chumba cha Ivory
S.L.P. 1994, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2866408, 2866376
Fax: +255 22 2865836, 2863496
Barua pepe: wildlife-division@twiga.com

# KUHUSU KITABU HIKI CHA MWONGOZO

**Kwanini Kitabu hiki kiliandikwa?**

Sera ya Wanyamapori Tanzania inatetea uanzishaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori kama njia ya kutekeleza shughuli za uhifadhi zilizoinjikwa kwenye jumuiya nchini Tanzania. Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori yanawakilisha maeneo mapya ya hifadhi yawanyamapori ambayo utawala wake utafanywa kwa ushirikiano kati ya Idara ya Wanyamapori, Halmashauri za Wilaya na taasisi nyingine katika sekta ya wanyamapori kama vile, Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Masuala ya Wanyamapori (TAWIRI). Katika jitihada hizi, pamoja na wajibu wao wa kuhifadhi wanyamapori, Maeneo haya yataendeshwa kama chombo cha biashara sambamba na mifumo mingine katika ardhi ya kijiji, kama itakavyoamuliwa na Mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji.

Kwa hiyo, Kitabu hiki ni nyenzo itakayoziwezesha jumuiya na watendaji katika maeneo haya ya majaribio ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori kufuata utaratibu wa utekelezaji kwa njia rahisi na yenye malengo maalum.

**Kitabu hiki kitawasaidia akina nani?**

Taarifa iliyomo katika Kitabu hiki inaweza ikawa na manufaa kwa watu wana aina tofauti ambao wana nia ya kuboresha juhudi za uhifadhi zilizoinjikwa katika jamii. Hadhira ya awali ni jumuiya zenyewe (watumiaji), halmashauri za wilaya, mashirika yasiyo ya kiserikali na watendaji wengine katika ngazi ya jumuiya. Taarifa iliyomo humu inaweza pia kuwa na manufaa kwa maafisa wa Wanyamapori, wataalam mbalimbali kutoka katika asasi zinazohusiana na mausuala ya wanyamapori na wawekezaji. Vile vile, taarifa iliyomo katika kitabu hiki inaweza kutumika kama mwongozo wa kutoa mafunzo katika ngazi zote katika utaratibu wa uanzishaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

**Kitabu hiki kinatoa taarifa gani?**

Kitabu hiki kinalenga kutoa kumbukumbu zilizoandikwa kwa lugha nyepesi na muundo rahisi mwepesi kwa ajili ya kusaidia katika utekelezaji wa Maeneo ya Jumuiya ya hifadhi ya Wanyamapori katika maeneo ya majaribio yaliyotengwa. Kinatoa mwongozo wenye mtiririko mfulululizo kuhusu jinsi ya kutekeleza masuala ya utambuaji, uanzishaji, na usimamizi wa Maeneo ya Jamii ya Hifadhi ya Wanyamapori pamoja na uhamasishaji wa wanavijiji kuhusu umuhimu wa maeneo haya. Kinatoa pia mwongozo kuhusu matumizi ya rasilimali, kugawana faida kati ya wadau mbalimbali na kuelezea kwa ufasaha jinsi ya kushughulia migogoro itakayoweza kutokea katika utekelezaji wa utaratibu mzima wa uanzishaji wa maeneo hayo.

**Jinsi ya kutumia kitabu hiki**

Kitabu hiki kinaweza kutumika kulingana na mahitaji ya msomaji. Watumiaji ambao wangependa kupata picha ya jumla kuhusu utaratibu wa kuanzisha maeneo ya jumuiya ya hifadhi ya wanyamapori, wanaweza kukisoma chote kwa mfulululizo. Wengine, ambao wako katika hatua fulani katika uanzishaji wa maeneo wanaweza kusoma sehemu fulani maalum tu na inapobidi kurejea kwenye sehemu nyingine.

# YALIYOMO


Orodha ya Yaliyomo (4)

Dibaji (5)

Orodha ya Vifupisho (6)

Tafsiri ya Dhana Muhimu (7)

Sehemu 1: Utangulizi (10)

Sehemu 2: Uanzishaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (11)

Sehemu 3: Utambuaji wa Miradi au Programu za Hifadhi iliokitwa katika Jumuiya (12)

Sehemu 4: Uanzishaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori katika Maeneo ya Jumuiya za Kimila (13)

Sehemu 5: Asasi, Miundo na Nyenzo za Kuendeshea Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (16)

Sehemu 6: Kutayarisha Mipango ya Matumizi ya Ardhi (20)

Sehemu 7: Maandalizi ya Mpango wa Utawala wa Jumla (22)

Sehemu 8: Utoaji wa Mamlaka kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya kuendesha shughuli za Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori (23)

Sehemu 9: Utoaji wa Hati ya Utumiaji kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa (25)

Sehemu 10: Uwekezaji na Ubia katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (26)

Sehemu 11: Utumiaji wa Rasilimali zilizopo katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori (29)

Sehemu 12: Faida, Mapato na Uchangiaji wa Gharama katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (33)

Sehemu 13: Asasi katika Usimamiaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (36)

Sehemu 14: Masuala ya Jumla yahusuyo Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (38)

Kutoa Kipaumbele Kijinsia (38)

Misaada kwa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (38)

Uinuaji wa Uwezo (39)

Uratibu wa Masuala yanayogusa Sekta Mbalimbali (40)

Utatuzi wa Migogoro na Usuluhishi (41)

Makosa ya Jinai na Adhabu (42)

# DIBAJI

Mwongozo wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori unatarajia kusaidia utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori Tanzania, 1998. Mwongozo huu ni maelekezo ya kiutawala ambayo lengo lake ni kusawazisha mambo ya kiutendaji ndani ya Kanuni za Hifadhi ya Wanyamapori (Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori), 2002. Kwa hiyo Mwongozo huu ni nyongeza tu ya hizo kanuni. Mwongozo huu unaweka wazi na bayana baadhi ya mambo yaliyomo ndani ya hizo Kanuni.

Kabla ya kuziandika hizo Kanuni, kulikuwepo na mashauriano mengi baina ya wadau mbalimbali. Ili kuyatendea haki mashauriano hayo na gharama kubwa iliyotumika katika kuanzisha dhana nzima na wazo la "Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyapori"(WMA), uandishi wa mwongozo huu, kwa kiwango kikubwa, umejumuisha maoni ya wadau mbalimbali na tafiti zilizofanyika. Jitihada kubwa imefanyika ili kuufanya mwongozo huu uweze kueleweka kiurahisi kwa watumiaji wote.

Mwongozo huu unatoa taratibu za uanzishaji Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) pamoja na jinsi ya kupata hadhi ya haki ya matumizi katika maeneo hayo. Asasi nyingi, pamoja na majukumu yake yamejumuishwa ndani ya mwongozo huu, ikiwa ni pamoja majukumu ya wadau wengine kama vile Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO's) na sekta binafsi.

Kwa kuwa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yataendeshwa kama maeneo ya uhifadhi na pia biashara, maeneo ya uwekezaji na ubia pia yameainishwa na kujumuishwa. Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yanahusisha wadau wengi katika usimamizi. Kwa mantiki hiyo yapo mahusiano yanayoingiliana kwa namna tofauti. Mwongozo huu unaangalia masuala ya ujumla katika kusimamia Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Kwa kuzingatia kwamba hifadhi yarasilimali za wanyamapori kwa kutumia wananchi wenyeji ni mtazamo mpya katika hifadhi ya wanyamapori Tanzania, inatarajiwa kwamba uzoefu wa wananchi hao utalazimisha kuboresha zaidi mwongozo huu. Kwa hiyo wadau wote wanaombwa kusaidia kuendeleza, kama walivyokwisha anza, kuifahamisha serikali juu ya maendeleo mapya ndani ya maeneo yao ili mwongozo huu uweze kuboreshwa ili kuendana na mahitaji halisi ya wakati husika. Kwa kuitikia wito huo, Mkurugenzi atatoa mwongozo mpya pale inapolazimu.

E.L.M. Severe
Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori
2003

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AA | Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa. |
| APU | Kikosi cha Kuzuia Ujangili |
| CBO | Chama cha Jumuiya |
| CITES | Mkataba wa Biashara ya Kimataifa ya aina za wanyama na mimea pori zilizoko hatarini kutoweka. |
| DBKO | Afisa wa Ufugaji Nyuki wa Wilaya |
| DC | Halmashauri ya Wilaya / Mkuu wa Wilaya |
| DCDO | Afisa wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya |
| DED | Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya |
| DFO | Afisa Misitu wa Wilaya |
| DFO | Afisa Uvuvi wa Wilaya |
| DGO | Afisa Wanyamapori wa Wilaya |
| DNRO | Afisa wa Maliasili wa Wilaya |
| EIA | Tathmini ya Athari ya Mazingira. |
| EPIQ | Sera ya Mazingira na Ukuzaji wa Asasi. |
| GMP | Mpango wa Jumla wa Usimamizi. |
| GOT | Serikali ya Tanzania. |
| GR | Mapori ya Akiba |
| LUP | Mpango wa Matumizi ya Ardhi |
| M &E | Ufuatiliaji na Tathmini |
| MNRT | Wizara ya Maliasili na Utalii |
| MRALG | Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. |
| NCA | Hifadhi ya Ngorongoro |
| NCAA | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro |
| NGO | Mashirika yasiyo ya Kiserikali. |
| NP | Hifadhi za Taifa |
| PA | Maeneo yaliyohifadhiwa Kisheria |
| PAC | Kudhibiti Wanyama waharibifu wa Mali na Maisha ya watu. |
| PRA | Mpango wa Ushirikishaji Vijijini. |
| RMZP | Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali. |
| TANAPA | Hifadhi za Taifa Tanzania |
| TAWIRI | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Wanyamapori |
| TWPF | Mfuko wa Kulinda Wanyamapori Tanzania |
| VEO | Afisa Mtendaji wa Kijiji |
| VGS | Askari Wanyamapori wa Kijiji |
| VLA | Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya 1999 |
| VNRC | Kamati ya Maliasili ya Kijiji |
| WCA | Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya 1974 |
| WD | Idara ya Wanyamapori |
| WDC | Kamati ya Maendeleo ya Kata |
| WMA | Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori |

# TAFSIRI YA DHANA MUHIMU

Katika mwongozo huu, ilimradi tu haipingani na Kanuni za Hifadhi yaWanyamapori katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori za mwaka 2002:-

*Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa (AA):* maana yake ni makundi yaliyoteuliwa na yaliyopewa mamlaka ya kusimamia wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa, Hifadhi ya Ngorongoro na Mapori ya Akiba.

*Afisa mwenye Mamlaka:* maana yake ni askari wanyamapori wa Kijiji wenye mamlaka kwa mujibu wa Kanuni.

*Faida:* maana yake ni vitu au fedha inayopatikana kutokana na uendeshaji na utawala wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

*Rasilimali za Kibiolojia:* maana yake ni rasilimali zenye uhai (mimea, wanyama pamoja na wadudu, pia viumbe vinavyoonekana kwa darubini) ziishizo duniani.

*Jumuiya:* maana yake ni Jumuiya ya watu wa mahali mipango ilipo, kama ilivyotafsiriwa kama uwepo wa raia wa Tanzania, wanaokaa katika eneo fulani.

*Kikundi cha Wanajumuiya:* maana yale ni kikundi ambacho lengo lake kuu ni kuhifadhi rasilimali kwa namna ambayo inachochea matumizi endelevu ya rasilimali kwa faida ya Jumuiya za mahali hapo.

*Gharama:* maana yake ni fedha, nafasi, ikolojia, huduma na gharama za kiJumuiya zinazojitokeza wakati wa mchakato wa kufanya shughuli fulani ndani ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

*Mkurugenzi wa Wanyamapori:* maana yake ni Mkuu wa Idara ya Wanyamapori ndani ya Wizara inayohusika na Wanyamapori katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Baraza la Wilaya la Ushauri wa Maswala ya Maliasili:* maana yake ni bodi ya ushauri iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 27, na inajumuisha Bodi ya Pamoja kati ya Wilaya na Wilaya ya Ushauri wa Rasilimali.

*Ukuaji wa ikolojia:* maana yake ni uwezo wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori kuendelea kuwa eneo endelevu la ikolojia na kwa matumizi yaliyotarajiwa.

## Tafsiri ya Dhana Muhimu Inaendelea ...

*Thamani ya Kiuchumi:* maana yake ni thamani ya kifedha ya rasilimali zilizoruhusiwa, matumizi ya uvunaji na yasiyo ya uvunaji wa moja kwa moja wa rasilimali, kama ambavyo itategemea tathmini ya faida na gharama.

*Askari Wanyamapori wa Serikali:* maana yake ni waajiriwa wa Serikali ya Tanzania wenye dhamana ya kulinda rasilimali za wanyamapori.

*Mwongozo:* Maana yake ni Mwongozo kuhusu Kuteuliwa kwa eneo kuwa la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori na Uendeshaji wa Eneo hilo.

*Baraza la Wilaya la Ushauri wa Masuala ya Maliasili:* maana yake ni Bodi ya Ushauri iliyoanzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 27 ambayo inahusisha Wilaya moja au zaidi ya moja kuhusu Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

*Kitega Uchumi:* maana yake ni mzunguko wa mtaji wa kuendeleza au kuboresha miundombinu na huduma katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori (WMA).

*Ubia:* maana yake ni makubaliano ya Mamlaka husika kati ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa na mtu au kampuni kufanya biashara fulani inayohusu au yenye mwingiliano na utawala au Hifadhi ya Wanyamapori katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

*Leseni:* maana yake ni ruhusa ya kimaandishi iliyotolewa na Mamlaka husika za Serikali kwa mujibu wa sheria za kutumia rasilimali.

*Waziri:* maana yake ni Waziri anayehusika na Uhifadhi wa Wanyamapori.

*Rasilimali zisizo za Kibiolojia:* maana yake ni rasilimali zote, isipokuwa rasilimali zenye uhai zilizopo au zenye thamani ya kiuchumi kwa jumuiya za mahali mipango ilipo, mfano; madini, maji, maeneo yenye mvuto n.k.

*Ushirikiano:* maana yake ni makubaliano baina ya Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa na mtu mwingine kwa mjibu wa vifungu vya Sheria ya Mikataba, (Sura ya 433) na Sheria ya Makampuni, (Sura ya 212), pamoja na sheria husika nyingine.

*Kibali:* maana yake ni ruhusa ya mamlaka iliyotolewa na Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kumruhusu mtu mwingine kufanya baadhi ya shughuli ndani ya Eneo la Jumuiya la Hifadhi yaWanyamapori.

*Kanuni:* maana yake ni Kanuni za Hifadhi ya Wanyamapori (Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori) za 2002.

## TAFSIRI YA DHANA MUHIMU Inaendelea ...

---

*Uhakika wa Umiliki katika Muda Uliowekwa:* maana yake ni muda ulioruhusiwa kwa eneo lililopewa hadhi ya Eneo la Jumuiya la Hifadhi yaWanyamapori, kuendelea kuwa hivyo.

*Mgawanyo:* maana yake ni ugawanaji wa faida, mapato na gharama zitokanazo na Jumuiya wanachama au wadau katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

*Uwingi wa Rasilimali za Wanyamapori:* maana yake ni rasilimali katika Eneo la Jumuiya la Uhaifadhi wa Wanyamapori zinazohusu uwingi, uanuwai na upekee wake katika kufikia kiwango cha chini kilichowekwa na Mkurungenzi wa Wanyamapori.

*Muda wa kumiliki Ardhi:* maana yake ni utumiaji au uhodhi wa ardhi.

*Jumuiya za Kimila:* maana yake ni Jumuiya ambazo hutegemea maliasili kwa ajili ya chakula chake kwa zaidi ya asilimia 75.

*Hati ya Utumiaji:* maana yake ni ruhusa ya kutumia rasilimali za wanyamapori zinazopatikana katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi yaWanyamapori kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

*Askari Wanyamapori wa Kijiji:* maana yake ni wanakijiji walioajiriwa na Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kulinda rasilimali za wanyamapori katika ardhi ya kijiji na ndani ya Eeneo la Jumuiya la Hifadhi yaWanyamapori.

*Ardhi ya Kijiji:* maana yake ni ardhi kama ilivyoelezewa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji, 1999, na kwa ajili ya hizi Kanuni, itajumuisha ardhi inayohodhiwa na kutumiwa na Jumuiya za Kimila.

*Kijiji:* maana yake ni kijiji kama kilivyoelezewa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, na itajumuisha maeneo ya Jumuiya za Kimila yaliyopewa hadhi hiyo na Mkurugenzi.

*Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori:* maana yake ni eneo lililotangazwa na Waziri liwe hivyo baada ya kutengwa na Serikali ya Kijiji kwa madhumuni ya Hifadhi ya Wanyamapori.

*Wanyamapori*: maana yake ni spishi za wanyama au mimea ya pori na ya kienyeji na makazi na mifumo ya ikolojia yake; hupatikana Tanzania na vile vile aina za kigeni zilizoingizwa nchini Tanzania na ambazo zimefungiwa mahali kwa muda kabla hazijaingizwa mwituni.

# SEHEMU 1: UTANGULIZI

## MSINGI WA KUANDIKA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu umetengenezwa chini ya Kanuni ya 78 ya Kanuni za Hifadhi ya Wanyamapori (Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori), 2002.

## MADHUMUNI LENGWA YA MWONGOZO

Mwongozo huu unatarajia kusaidia utekelezaji wa Kanuni na kuchochea matarajio ya Sera ya Wanyamapori ya Tanzania, 1998.

Kanuni za Hifadhi ya Wanyamapori (Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori), 2002 zilizotengenezwa chini ya vifungu vya 19 na 84 vya Sheria ya Hifadhi Wanyamapori ya 1974, pamoja na mwongozo huu, vinalenga katika kuwawezesha wananchi waishio vijijini kushiriki katika utunzaji na utumiaji wa rasilimali za wanyamapori ndani ya ardhi ya vijiji vyao.

## MAKUSUDIO YA SERA YA WANYAMAPORI YA TANZANIA, 1998

Sera ya Wanyamapori ya Tanzania inakusudia:

- Kukuza Uhifadhi wanyamapori na makazi yao katika maeneo yaliyo nje ya maeneo kiini kwa Uhifadhi Wanyamapori yaliyotengwa mahsusi na sheria kwa kuanzisha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori;

- Kuhamishia usimamizi wa maeneo hayo ya Jumuiya kwa wananchi vijijini na hivyo basi kuulinda ushoroba wa wanyama, njia za uhamiaji, maeneo ya usalama wa wanyama, na kuhakikisha kwamba Jumuiya zilizo katika maeneo hayo ya wanyama zinafaidika vilivyo kutokana na uhifadhi wanyamapori;

- Kuhakikisha kwamba wanyamapori wanathaminiwa inavyositahili ili kupunguza matumizi haramu na kuhimiza matumizi endelevu katika Jumuiya za vijiji;

- Kuweka na kuwezesha kuwepo kwa mazingira ambayo yatahakikisha kwamba mipango endelevu na halali ya shughuli za wanyamapori inazifaidisha moja kwa moja jumuiya za mahali mipango hiyo ilipo.

# SEHEMU 2: UANZISHAJI WA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI

## UHAMASISHAJI NA UELEWESHAJI WA JUMUIYA

Kabla hawajaamua kama wanataka kuanzisha Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori, vijiji vinahitaji kuhamasishwa na kueleweshwa kuhusu umuhimu, gharama na faida za kutunza rasilmali za wanyamapori, taratibu za kufuata ili kupewa hadhi ya maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori pamoja na haki na dhima zao.

Idara ya Wanyamapori ikishirikiana na mashirika mengine yanayojihusisha na wanyamapori kama vile TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Halmashauri za Wilaya zitaendesha vipindi vya uhamasishaji wa wanavijiji.

### TARATIBU ZA KUFUATA KABLA YA KUFANYA UHAMASISHAJI

Kikundi cha uhamasishaji kitatimiza na kufuata taratibu zifuatazo:

- Kupata ruhusa maalumu ya kimaandishi kutoka mamlaka husika za Wilaya
- Kushirikiana na tawala za Kata na Vijiji
- Kufanya mkutano na wanakiijiji wote, kwa kupitia Halmashauri ya Kijiji, na kuwaelezea wanakijiji malengo, faida na gharama za kuanzisha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori pamoja na kuwafahamisha thamani ya rasilimali ya wanyamapori katika eneo hilo.
- Kutumia njia nyingine kama video, ngoma, nyimbo, maigizo, vipeperushi, majarida n.k.
- Kulenga kundi fulani la Jumuiya kama vile, watoto wa shule, wazee, wanawake, vijana, wawindaji, viongozi wa serikali za mitaa na wanasiasa.
- Kusikiliza maoni ya wanakijiji kupitia mikutano yao ya wanakijiji.

# SEHEMU 3: TARATIBU ZA KUTEUA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI

Kabla eneo halijateuliwa kuwa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, ni lazima taratibu zifuatazo zifuatwe:

1. Halmashauri ya Kijiji itatoa mapendekezo kwa Mkutano Mkuu wa Kijiji kuhusu sehemu ya ardhi ya kijiji husika inayostahili kuwa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

2. Chama Wakilishi cha Jumuiya kilichoidhinishwa (AA) kitawasilisha maombi kwa niaba ya vijiji kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori yakiambatana na nyaraka zifuatazo:

    - Nakala iliyothibitishwa ya kumbukumbu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji kuidhinisha kuteuliwa kwa eneo husika; na kumbukumbu hiyo lazima iwe imeshuhudiwa na Afisa aliyeruhusiwa kisheria kupokea viapo na shuhuda
    - Taarifa kamili kuhusu yale yaliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni
    - Nakala ya cheti cha usajili wa Chama cha Jumuiya na nakala hiyo lazima iwe imeshuhudiwa na Afisa aliyeruhusiwa na sheria kupokea viapo na shuhuda
    - Mpango wa Kijiji wa Matumizi ya Ardhi ulioidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji husika.
    - Rasimu za Mpango wa Jumla wa Usimamizi au Mpango wa Kanda wa Usimamiaji wa Rasilimali

3. Mkurugenzi atakusanya taarifa juu ya eneo linalotarajiwa kuwa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori zitakazojumuisha yafuatayo:

    - Jina la Eneo
    - Fedha kwa ajili ya kuendeshea eneo
    - Vitega uchumu (kama vipo)
    - Shughuli za Kiuchumu (kama zipo)
    - Shughuli za Maendeleo (kama zipo)
    - Watendaji katika mradi au programu

# SEHEMU 4: UANZISHAJI WA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI KATIKA MAENEO YA JUMUIYA ZA KIMILA

## VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KUANZISHA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI

Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yanaweza kuanzishwa katika maeneo yafutayo:

- Maeneo yaliyo nje ya Maeneo mahsusi yaliyohifadhiwa kisheria kwa ajili ya uhifadhi wanyamapori
- Maeneo yanayotumiwa na jamii asilia katika eneo husika
- Maeneo yaliyo ndani ya ardhi ya kijiji/vijiji husika

Hakuna sehemu yoyote itakayotengwa kuwa Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori bila ya kutimiza vigezo vyote vifuatavyo:

- Kuwa na raslimali ya kutosha na inayoweza kuvunwa
- Maliasili yake iwe ina thamani ya kuridhisha kiuchumi
- Iwe toshelevu ki-ikolojia au iwe katika sehemu ya ikolojia iliyo toshelevu
- Kwa mujibu wa sheria inayoratibu ardhi ya vijiji, eneo husika liwe ni sehemu ya raslimali ya kijiji kimoja au zaidi ya kijiji kimoja

## Dhima ya halmashauri ya Wilaya:

Ili kuwezesha mfumo wa uanzishaji wa maeneo haya, Halmashauri ya Wilaya ikishirikiana na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori watafanya yafutayo:

- Ainisha watu waishio ndani ya jumuiya za kimila
- Anzisha na kutunza orodha ya hizo jumuiya za kimila zikionyesha:
  - Mahali
  - Idadi ya Watu
  - Makadirio ya eneo lote linalotumika na jumuiya mahsusi
  - Makadirio ya ukubwa wa eneo
  - Asilimia tegemezi ya rasilimali za asili
  - Muundo wa uongozi wa jumuiya

| ENEO | MAHALI | IDADI YA WATU | MAKADIRIO YA UKUBWA WA ENEO LOTE | MAKADIRIO YA UKUBWA HALISI WA ENEO |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

Mfano wa ukurasa wenye kumbukumbu za maeneo ya jumuiya za kimila

### Dhima ya Halmashauri ya Wilaya inaendelea...

- Andaa na kutuma kwa Mkurugenzi, fomu yenye habari za uhakika ikionyesha vigezo muhimu vya eneo kupewa hadhi ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, chini ya Kanuni ya 11.
- Pendekeza kwa Mkurugezi eneo zuri linalofaa kuanzishwa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa matumizi ya Jumuiya za kimila.

## Uteuzi wa Maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori KWA matumizi ya JAMII ZA KIMILA

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa na Halmashauri ya Wilaya, **Mkurugenzi** atafanya yafuatayo:

- Atayapa hadhi Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa matumizi pekee ya Jumuiya hiyo chini ya Kanuni ya 12(3)
- Atapendekeza kwa Waziri eneo lililopewa hadhi ya kuwa Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori kwa Jumuiya za Kimila.

## Kukubaliwa au Kukataliwa na Rufaa

**Mkurugenzi** wa Wanyamapori, mara apatapo ombi la kutengwa kwa eneo kuwa Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori, atalazimika kumtaarifu aliyeomba iwapo ombi lake limekubaliwa au limekataliwa.

**Mkurugenzi** anaweza kulifikiria tena ombi lililokataliwa, pale ambapo ombi hilo litakuwa limerekebishwa ili lizingatie maelekezo yoyote ambayo yatakuwa yametolewa.

## KUTANGAZWA RASMI KWA ENEO LA JUMUIYA LA HIFADHI YA WANYAMAPORI NA CHAMA WAKILISHI CHA JUMUIYA

Baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Mkurugenzi **Waziri** atafanya yafutayo:

- Ataruhusu kutangazwa kwa eneo lililopewa hadhi ya Eneo la Jumuiya ya Hifadhi wa Wanyamapori kwa Jumuiya za kimila kwa mujibu wa Kanuni ya 16 (3).
- Atatoa hati ya Kuteua Kikundi cha Jumuiya kuendesha na kusimamia shughuli za wanyamapori eneo lililoteuliwa kama ilivyoidhinishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni.
- Ataidhinisha kuchapishwa kwa pamoja katika Gazeti la Serikali kwa Vyama Wakilishi na Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yalioanzishwa na Jumuiya za kimila zitatumiwa na Jumuiya hizo kulingana na mila na desturi zao, ilimradi hizo mila na desturi hazipingani na Kanuni.

# *Kumbukumbu ya Haraka Haraka!*

## Uanzishaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori utafuata hatua zifuatazo:




Taratibu za kupata hadhi ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori

## SEHEMU 5: ASASI, MIUNDO NA NYENZO ZA KUENDESHEA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI

Ili kusimamia maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa ufanisi, ni lazima wanavijiji wawe tayari kutambua asasi zitakazohusika, kutengeneza miundo na kutayarisha nyenzo zitakazorahisisha usimamiaji wa maeneo haya. Muundo ulioonyeshwa hapa chini unaonyesha ardhi iliyotengwa na vijiji 19 vilivyo jirani kwa ajili ya kuanzisha eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori.




Kielelezo kuonyesha Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori lililoanzishwa na vijiji 19 (Mfano wa JUKUMU)

Kabla ya kuanza kushughulikia miundo na nyenzo, kuna mambo matatu ambayo ni lazima wanavijiji wayatekeleze:

**1** **Kuunda Chama Wakilishi cha Jumuiya** ambacho kitaidhinishwa na Mkurugenzi wa Wanyamapori kusimamia wanyamapori katika ardhi ya kijiji. Idara ya Wanyamapori, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, TANAPA, Halmashauri ya Wilaya au Shirika lisilo la Kiserikali vitasaidia kutayarisha mkutano wa Baraza la Wanavijiji kwa ajili ya kuwahamasisha wanavijiji na kuwaongoza katika uundaji wa Chama Wakilishi cha Jumuiya. Wanavijiji waliohamasishwa watachagua wawakilishi ambao watakuwa na nafasi mbalimbali za uongozi katika Chama Wakilishi cha Jumuiya.

Ufuatao hapa chini ni mfano wa muundo unaoweza kusaidia kutoa mwongozo wakati wa kuunda vikundi na miundo vya kusimamia maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

**VIJIJI**

↓

Asasi: **[H]AURI YA CHAMA WAKILISHI CHA JUMUIYA**

Wajumbe: [...]na 3 kutoka katika mkutano mkuu wa [...] kinachoshiriki (v1, v2, v3….v18, v19)

Majukumu: *Kuajiri Askari Wanyamapori wa Kijiji ambao watalinda [...] Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori (WMA) [...]taarifa kwenye vijiji husika kuhusu uamuzi [...]ote utakaochukuliwa na Halmashauri.*

↓

**KAMATI KUU YA CHAMA WAKILISHI CHA JUMUIYA**

Wajumbe: [...]10 watakaochaguliwa kutoka kwenye [...]nashauri ya Chama Wakilishi kilichoidhinishwa

Majukumu: *Kutekeleza kwa vitendo shughuli zote zitakazoamuliwa na Halmashauri ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa*

↓

Asasi: **[B]ODI YA CHAMA WAKILISHI KILICHOIDHINISHWA**

Wajumbe: [...]ıbe 5 kutoka Kamati Kuu ya Chama [...]shi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa

Majukumu: *[...]li Wadhamini na kuingia mikataba na wawekezaji*

**Muundo wa Uendeshaji wa Chama Wakilishi cha Jumuiya (Mfano wa JUKUMU)**

**2** **Kuandaa Katiba.** Halmashauri ya Wilaya itawaongoza wanajumuiya/wanakijiji kuhusu jinsi ya kuandaa katiba. Pamoja na mambo mengine, Katiba itaonyesha yafuatayo:

- Jina
- Mipaka
- Ukubwa
- Mahali

## Maelezo mengine yaliyomo katika Katiba:

- Malengo ya Kikundi au Chama Wakilishi cha Jumuiya
- Majina ya Vijiji wanachama pamoja na Wilaya zao
- Masharti au sifa ya uanachama
- Maelezo kuhusu Viongozi ikiwa ni pamoja na:
  - Masharti au sifa za uongozi
  - Muda wa Uongozi
  - Masharti na taratibu za kubadili muda wa viongozi
  - Namna ya Uwakilishi
- Uwajibikaji wa Chama Wakilishi cha Jumuiya kwa wanakijiji, Halmashauri za Vijiji na mawasiliano na Halmashauri ya/za Wilaya
- Dhima za ngazi mbalimbali za Chama Wakilishi cha Jumuiya
- Uhusiano kati ya Chama Wakilishi cha Jumuiya na Halmashauri ya Kijiji
- Utawala na Utunzaji wa fedha
- Njia za kutatua migogoro ndani ya Chama Wakilishi cha Jumuiya
- Mpango wa maadili na hatua za kinidhamu

- Masharti ya maombi ya kusajiliwa kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya kulingana na Sheria ya Kanuni za Jumuiya (Maombi ya Usajili) za 1994 [Kanuni ya 4(1)] [Angalia Jedwali la kwanza kwenye Kanuni]

- Dhima ya Halmashauri za Vijiji kutoa mapendekezo ya kuanzisha sheria ndogo ndogo.

## 3 Kutayarisha Mpango wa Kimkakati (Strategic Plan)

Hatua inayofuata ni kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya kutayarisha mpango wa kimkakati ambao utajumuisha taarifa zifutazo:

- Dira
- Azma
- Malengo
- Majukumu na Shughuli
- Matarajio
- Mbinu za Ufuatiliaji & Tathmini
- Kupanga Mipango Mipya

Ni lazima Mpango wa Kimkakati uliotayarishwa uidhinishwe na Baraza la Wanavijiji.

# Sehemu 6: Kutayarisha Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Halmashauri za Vijiji zitaandaa mpango wa matumizi ya ardhi kulingana na vifungu vilivyoainishwa katika Jedwali la Sita la Kanuni.

Zoezi hili litajumuisha hatua za kutathmini, pamoja na kupendekeza matumizi endelevu na mbadala ya ardhi vijijini ili kulinda bioanuwai na kuendeleza maisha bora kwa wanavijiji.

Utayarishaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi utaongozwa na taratibu zifuatazo:

1. Halmashauri ya Kijiji itapendekeza kwenye Mkutano Mkuu wa Wanakijiji, sehemu ya ardhi ya kijiji itakayotengwa kama "sehemu ya jumla ya kijiji" kwa ajili ya kuanzisha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori. (Rejea kifungu cha 13 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999).

2. Baraza Kuu la Kijiji litatoa uamuzi juu ya mapendekezo ya mipango ya matumizi ya ardhi. (Rejea kifungu cha 13 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999).

# Baada ya kutayarisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji…

☞ Halmashauri ya Kijiji itanakiri uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Wanakijiji wa kutenga eneo fulani kwa matumizi ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ndani ya "Daftari la Umma la mambo ya Ardhi" (Rejea Kanuni ya 39 ya Kanuni za Ardhi za Vijiji, za 2001).

☞ Pale ambapo Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori inayotaka kuanzishwa ipo ndani ya himaya ya vijijii mbalimbali, vijiji hivyo itabidi vikubaliane kuanzisha "Mpango wa Pamoja wa Matumizi ya Ardhi". (Rejea: kifungu cha 11 cha Sheria ya Ardhi ya vijiji, 1999: Sehemu ya IV ya Kanuni za Ardhi ya Vijijini za 2001: Angalia Kanuni ya 35 na Jedwali la Sita kwenye Kanuni za Uhifadhi Wanyamapori (Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori) za 2002.

☞ Halmashauri ya Wilaya itashauri na kutoa maelekezo kwenye Halmashauri ya Kijiji. (Rejea: Kifungu cha 9 na 13 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji 1999)

☞ Mpango wa Matumizi ya ardhi wa kuanzisha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori utafuatiwa na hatua kama zilivyoainishwa katika mwongozo wa ushirikishwaji katika utawala wa mipango ya matumizi ya Ardhi ya Tanzania (Rejea: Mwongozo wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, Sura ya 2.7 kadi D, Boxi la 4.1)

☞ Tathmini ya Athari katika Mazingira (EIA), itafanyika katika kila mpango wa matumizi ya ardhi.

☞ Katika kushughulikia maswala yanayohusu wanyamapori, Halmashauri ya Kijiji itakuwa na dhima ya kuonana na kuchukua maoni ya Mkurugenzi au Mamlaka za Wanyamapori, na ikibidi

Halmashauri ya Kijiji itatekeleza uamuzi wao. (Rejea: vifungu vya 7 na 8 vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999).

# SEHEMU 7: MAANDALIZI YA MPANGO WA JUMLA WA USIMAMIZI

Chama Wakilishi cha Jumuiya kinatakiwa kutayarisha Mpango wa Jumla wa Usimamizi kulingana na vifungu vilivyoainishwa katika Jedwali la Saba la Kanuni hizi.

Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa rasilimali utaainisha matumizi mbalimbali na usimamiaji wa rasilimali kwa nia ya kuboresha mazingira na kuhakikisha mafao ya kiuchumi kwa wadau husika.

Kama hatua za muda, Chama Wakilishi Cha Jumuiya kilichoidhinishwa kinaweza kuandaa Mpango wa Kanda wa Usimamiaji wa Rasilimali katika sehemu fulani, kwa kufuatana na utaratibu ulivyoelezwa ndani ya Jedwali la Nane kwenye Kanuni. Utaratibu huo utadumu kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ulioidhinishwa. (Rejea Kanuni ya 36).

**Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa Mpango wa Jumla wa Usimamizi:**

1. Tumia fomu iliyoainishwa ndani ya Jedwali la Saba kwenye Kanuni.
2. Tafuta msaada wa kitaalamu kutoka kwenye Mamlaka za Wanyamapori.
3. Shirikisha wadau muhimu.

Baada ya Mpango kuandaliwa, Chama Wakilishi cha Jumuiya kitawasilisha Mpango wa Jumla wa Usimamizi au Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali katika sehemu fulani kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori kwa ajili ya kuidhinishwa.

# Sehemu 8: Utoaji wa Mamlaka kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya kuendesha shughuli za Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori

## Nani anatakiwa kuwasilisha ombi?

Maombi ya Chama Wakilishi cha Jumuiya kuwa Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa yatachukuliwa kama vile pia ni maombi ya kupewa hadhi ya kuwa Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori chini ya Kanuni ya 13.

## Mahitaji muhimu ni yapi?

Chama Wakilishi cha Jumuiya inaweza kupewa mamlaka ya kusimamia rasilimali za maliasili katika ardhi ya kijiji baada ya kutimiza mambo yafuatayo:

1. Kukisajili Chama Wakilishi cha Jumuiya chini ya "Societies Ordinance. Cap. 337".

2. Kusajili wadhamini wa kikundi hicho chini ya Sheria ya Uandikishwaji Udhamini, Sura ya 375.

3. Kuwasilisha maombi ya Kikundi au Ushirika wa wanajumuiya kwa Mkurugenzi, ili kiruhusiwe kusimamia Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

**Maombi yataambatanishwa na nyaraka zifuatazo:**

- Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kijiji ambao ulipitisha uamuzi wa uundwaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori,
- Fomu iliyokamilika yenye vigezo muhimu juu ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori, kama inavyopatikana katika Jedwali la Pili kwenye Kanuni.
- Nakala iliyothibitishwa ya Cheti cha kusajiliwa Chama Wakilishi cha Jumuiya.
- Nakala ya Katiba ya Chama Wakilishi cha Jumuiya.
- Mpango wa Matumizi ya Ardhi uliopitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji au Vijiji
- Ramani ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori iliyopendekezwa ikiambatana na Mpango wa Matumizi ya Ardhi.
- Maelezo ya mipaka, ukubwa na jina la Maeneo hayo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.
- Nakala ya rasmu ya Mpango wa Jumla au Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Raslimali wa eneo hilo.

**4** Kutuma Maombi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori

**5** Kupeleka Nakala za maombi kwenye Halmashauri ya Wilaya husika.

## UTARATIBU WA KUKUBALI MAOMBI

**1** Mkurugenzi atapendekeza kwa Waziri, Chama Wakilishi cha Jumuiya kilichotimiza masharti yote kitangazwe kuwa “Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa” kuendesha Eneo la Jumuiya la uhifadhi.

**2** Waziri atatoa Cheti cha mamlaka kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya kulingana na Kanuni ya 16(2) na utaratibu ulivyoelezwa katika Jedwali la 3 kwenye Kanuni.

**3** Tangazo la Chama Wakilishi cha Jumuiya kuwa chama kilichopewa mamlaka litachapishwa katika Gazeti la Serikali.

# Sehemu 9: Utoaji wa Hati ya Utumiaji kwa Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa

## Masharti ya kutoa Hati ya Utumiaji

Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa na kupewa 'Cheti' cha mamlaka kuwa Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa, hakitakuwa na haki ya kutumia rasilimali za wanyamapori katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori, mpaka hapo Chama hiki kitakapoomba na kupewa 'Haki ya Utumiaji' kutoka kwa Mkurugenzi kulingana na Kanuni ya 39(1) na kama ilivyoainishwa katika Jedwali la 10 kwenye Kanuni.

Hati ya utumiaji wa rasilimali za wanyamapori itatolewa kwa mujibu wa Mpango wa Jumla au Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali katika eneo fulani au taarifa nyingine yoyote Mkurugenzi atakayoona inafaa. Haki za utumiaji wa rasilimali za wanyamapori hazihamishiki.

### MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WENYE HATI MAALUM ZA UTUMIAJI

Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa chenye 'haki ya utumiaji' kitakuwa na mamlaka ya kuingia mikataba ya uwekezaji na mwekezaji au wawekezaji katika kutumia rasilimali hizo za wanyamapori katika Maeneo ya jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori.

Mikataba au makubaliano kwa niaba ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa ni lazima yasainiwe na wadhamini waliosajiliwa ambao pia wameruhusiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Katiba husika ya Chama Wakilishi cha Jumuiya.

Mikataba na Makubaliano hayatahusisha usimamiaji wa maliasili na utengaji wa maeneo ya kuwinda katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori.

## Kusitisha na kurejesha Haki ya utumiaji

Mkurugenzi anaweza kusitisha Haki ya utumiaji muda wowote kwa sababu maalum inayoelezeka. Chama Wakilishi cha jumuiya kilichoidhinishwa kinaweza kurejesha Haki ya Utumiaji kwa ridhaa yake lakini kufanya hivyo kutawezekana tu baada ya kupitishwa na Baraza kuu la Kijiji na baada ya hapo Chama Wakilishi cha Jumuiya kilichoidhinishwa ni lazima kiheshimu uamuzi huo.

# Sehemu 10: Uwekezaji na Ubia katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

## Masharti ya Jumla ya Uwekezaji na Ubia katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

Makubaliano ya uwekezaji na miradi ya maendeleo katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi yaWanyamapori yatakuwa kwa kipindi cha miaka mitatu tu na kipindi hiki kinaweza kikaongezwa tena baada ya miaka hiyo kumalizika.

Pale uwekezaji au miradi ya maendeleo katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori itafanywa na Chama Wakilishi cha Jumuiya utahusisha pia matumizi na umilikaji wa ardhi, basi vifungu vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji, 1999 itatumika.

Makubaliano ya uwekezaji katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori yatafanyika kulingana na Jedwali namba 12 ya kanuni hizi. Nakala ya makubaliano hayo itatumwa kwenye Halmashauri ya Wilaya na kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.

## Nani anastahili kuwekeza katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori ?

Uwekezaji katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori utafanyika kwa lengo la kutumia rasilimali zitokanazo na wanyamapori, na uwekezaji huo utafanywa na wafuatao:

- Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa chenye haki ya utumiaji.
- Mwekezaji mwenye mkataba wa Uwekezaji na Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa.
- Mwekezaji mwenye mkataba wa Ubia na Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa (Rejea Kanuni ya 39, Sehemu VIII ya Kanuni na Jedwali la 12).

## Masharti Maalum ya Uwekezaji na Ubia

- Vitega uchumi vyote ni lazima vizingatie Tathmini ya Athari katika Mazingira, na viendane na Mpango wa Jumla wa Usimamizi au Mpango wa Kanda wa matumizi ya rasilimali wa eneo husika.

- Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili itatoa mwongozo na ushauri kwa Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa juu ya mambo yahusuyo makubaliano, mikataba, vitega uchumi na maendeleo ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

- Mikataba ya Ubia na ya Uwekezaji haitahusisha utawala na ulinzi wa maliasili au ugawaji wa vitalu vya kuwinda.

- Mikataba ya uwekezaji itafuata utaratibu ulioainishwa katika Jedwali la 12 la Kanuni.

## Dhima ya Halmashauri ya Wilaya kuhusu Uwekezaji na Ubia katika maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

Mkataba wa Uwekezaji ambao utaendeleza ardhi ya kijiji kwa ajili ya matumizi halisi ya ardhi na umiliki wake na mwekezaji, utaungwa mkono na kupewa hati ya umilikaji wa ardhi na Halmashauri ya Kijiji husika, chini ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999.

Halmashauri ya kijiji inaweza kutoa Hati Miliki ya Ardhi ya Kimila kwa Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa ili kukiwezesha kutoa haki itokanayo na hiyo Hati Miliki kwa Mwekezaji.

Halmashauri ya Kijiji itakiwezesha Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa na mwekezaji kupata cheti cha Hati ya Ardhi ya Kimila, pamoja na hati zitokanazo na hiyo, ili kurahisisha uwezo wa huduma za kifedha katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori.

## Masuala ya Kisheria

Makubaliano ya Ubia yataongozwa na Sheria zifuatazo:

- Sheria ya Makampuni (Sura ya 212)
- Sheria ya Mikataba (Sura ya 443)
- Sheria ya Ardhi ya Kijiji, 1999
- Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya 1982
- Sheria nyinginezo husika

## Kamati ya Usimamizi wa Ubia

Kamati ya Usimamizi wa Ubia itaundwa kama chombo cha pamoja kitakachohusika na usimamizi wa shughuli za ubia katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori. (Rejea Kanuni ya 65)

Wajumbe wasiozidi wawili watatoka katika vikundi vifuatavyo:

- Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa
- Shirika au Kampuni
- Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili

Kamati ya Usimamizi wa Uwekezaji na Ubia itatayarisha kanuni zake yenyewe na utaratibu wake kwa ajili ya kuendesha mikutano yake.

Hakuna makubaliano ya uwekezaji au Mkataba wa Uwekezaji wa Ubia utakaoruhusiwa kutekelezwa bila ya kwanza kupata kibali cha Mkurugenzi.

## Upangaji wa Viwango vya Ada

Viwango vya ada vitatungwa na Waziri wa Maliasili na Utalii.

Wahusika kwenye mkataba wa uwekezaji yaani Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa, na Mwekezaji, watakuwa huru kushauriana na kukubaliana kuhusu viwango vya ada vilivyopangwa.

# Sehemu 11: Utumiaji wa Rasilimali zilizopo katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori

Matumizi ya rasilimali chini ya mwongozo huu yatahusisha 'matumizi yanayovuna' na au 'yasiyovuna' rasilimali za kibiolojia na zisizo za kibiolojia kwa namna ambayo haitaathiri mkakati wa ekolojia wa mzunguko wa maisha wa viumbe hai hao, kwa ajili ya Jumuiya katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori na hifadhi ya uanuwai wa kibiolojia.

Matumizi ya rasilimali zilizopo katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori mbali na nyama, yatakuwa kwa mujibu wa sheria za sekta husika.

Afisa Leseni anaweza kutoa leseni au kibali cha kukamata wanyama kwa watu wenye kibali kinachowaruhusu kutumia rasilimali za wanyamapori katika Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori.

## Matumizi yanayoruhusiwa ya rasilimali za wanyamapori

Uwindaji kwa ajili ya nyama kwa Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa, chini ya Kanuni ya 51.

Uwindaji wa wakazi wa eneo, chini ya Kanuni ya 52.

# Matumizi mengine yanayoruhusiwa

Utalii wa uwindaji chini ya Kanuni ya 53.

Utalii usiovuna rasilimali za wanyamapori, chini ya Kanuni ya 61.

Kukamata wanyama wakiwa hai, chini ya Kanuni ya 56.

# Matumizi yenye Masharti ndani ya Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori

Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kinaweza kutoa kibali cha matumizi yafuatayo kwa kuzingatia masharti ya leseni iliyotolewa na mamlaka husika:

**Mazao ya Misitu (miti) chini ya Kanuni ya 58 (Rejea Sheria ya Misitu ya 2002)**

**Rasilimali ya Nyuki chini ya Kanuni ya 59 (Rejea: Sheria ya Nyuki ya 2002)**

**Rasilimali za Samaki chini ya Kanuni ya 60 (Rejea: Sheria ya Samaki ya 1970)**

# Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori

**Uchimbaji madini, kwa mujibu wa Kanuni ya 62 (Rejea: Sheria ya Madini ya 1998)**

**Kuvuna wanyamapori**

**Ufugaji wa wanyamapori au katika uwanda (ranchi) kwa madhumuni ya kuingia katika biashara ya wanyamapori**

# Sehemu 12: Faida, Mapato na Uchangiaji wa gharama katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

## Walengwa Wakuu wa Manufaa yatokanayo na Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori

Faida, mapato na uchangiaji wa gharama ndani ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) utafuata Kanuni ya 73, 74 na 75.

Walengwa wakuu watakaofaidika na Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori ni wanakijiji katika kijiji au vijiji vitakavyounda Chama Wakilishi Cha Jumuiya.

Wadau wengine katika Faida, Mapato na Uchangiaji Gharama za kusimamia Eneo la Jumuiya la Uhifadhi ya Wanyamapori ni pamoja na Halmashauri za Wilaya, Hazina, Idara ya Wanyamapori, Hifadhi za Taifa Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa, Mfuko wa Kulinda Wanyamapori Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania na wawekezaji.

## Dhima ya Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa

- Ni dhima ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kusimamia mapato ya fedha yatokanayo na aina mbalimbali za matumizi ya rasilimali katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori (WMA). Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kitaongozwa na Kanuni ya 73(2) juu ya matumizi ya mapato yote kwa ujumla.

- Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kwa kushirikiana na Halmashauri ya kijiji vitahakikisha kwamba matumizi ya faida za pamoja yanalenga mikakati ya uchumi na kupunguza umasikini.

- Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kinatakiwa kuandaa 'Bajeti ya Mwaka' na 'Mpango wa Utekelezaji' mwanzoni mwa kila mwaka wa fedha.

- Bajeti hii na Mpango wa Utekelezaji vitawasilishwa kwenye Halmashauri ya Kijiji, ambayo nayo itavipeleka kwenye mkutano Mkuu wa Kijiji ili kupata idhini.

- Ili kutekeleza azma na malengo chini ya Faida, Mapato na Uchangiaji Gharama wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori, Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kitawajibika kufanya yafuatayo:

  - Kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa mwaka

  - Kufuata hatua na taratibu za kugawa fedha, kulipa kodi, madeni, na michango mingine kulingana na mpango mzima wa utendaji.

  - Kufungua akaunti ya benki na kuhakikisha makusanyo ya fedha yanapelekwa benki haraka iwezekanavyo.

  - Kutunza vitabu vya uhasibu.

  - Kuhakikisha vijiji wanachama vinapata taarifa ya fedha ya robo, nusu na ya mwaka, kupitia ofisi zake na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

## JE, ITAKUWAJE ENEO LA JUMUIYA LA HIFADHI YA WANYAMAPORI LIKIHUSISHA ZAIDI YA WILAYA MOJA?

Pale ambapo WMA inajumuisha wilaya zaidi ya moja, ni wajibu wa Bodi ya Pamoja ya Wilaya hizo ya ushauri wa maliasili kushauri na kutoa maelekezo juu ya uandaaji wa bajeti ya mwaka na mipango ya kiutendaji ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa.

# SEHEMU13: ASASI KATIKA USIMAMIAJI WA MAENEO YA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMAPORI

Asasi zenye dhima ya kusimamia Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori chini ya Kanuni ni:

- Vyama Wakilishi vya Jumuiya Vilivyoidhinishwa
- Halmashauri za Vijiji
- Mikutano Mikuu ya wanakijiji
- Halmashauri za Wilaya
- Bodi za Wilaya za Ushauri wa Maliasili
- Idara ya Wanyamapori
- Wizara ya Maliasili na Utalii
- TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngoronogoro na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania,
- Mashirika yasiyo ya Kiserikali
- Wawekezaji Binafsi

## DHIMA NA WAJIBU WA ASASI NYINGINE

### Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanaweza kutoa msaada wa kifedha au ufundi kwa Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa baada ya kupata ruhusa ya Waziri kwa mjibu wa mapendekezo ya Mkurugenzi (Rejea: Kanuni ya 77). Mashirika yasiyo ya kiserikali yana dhima au wajibu ufuatao:

- Kusaidia uanzishwaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa kushirikiana na Mkurugenzi, Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, viongozi wa Mapori ya Akiba na Hifadhi za Taifa, pamoja na Halmashauri za Wilaya.

- Kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri za wilaya katika kuhamasisha Jumuiya ili waunde WMAs.

- Kusaidia uundwaji wa Chama Wakilishi cha Jumuiya.
- Kusaidia vijiji kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi na Mpango wa Jumla.
- Kusaidia uandaaji wa sheria ndogo ndogo.

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kwa kushirikiana na Mkurugenzi na Halmashauri za Wilaya.

- Kufanya mambo yanayosaidia kujenga uwezo (utawala wa fedha; mpango wa utendaji wa mwaka; ukaguzi wa fedha; mpango maalum na kutoa kipaumbele mambo ya jinsia).

- Kushiriki katika Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili pale yanapoalikwa.

- Kushirikiana na mamlaka za wanyamapori katika kuangalia rasilimali.

## Sekta Binafsi

Dhima ya Sekta Binafsi kuhusiana na uendeshaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori inahusu maeneo ya uwekezaji, uendelezaji na masoko, ulinzi wa maliasili, kubadilishana mawazo na ulipaji wa kodi.

Hususan, sekta binafsi inashiriki katika uendeshaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kwa njia zifuatazo:

- Kuingia mkataba kama wawekezaji kuhusu matumizi ya rasilimali katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapor na Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa chini ya Kanuni ya 63.
- Kuingia makubaliano ya Ubia chini ya Kanuni ya 64.
- Kuuza na kupanua masoko ya rasilimali za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kulingana na Kanuni.
- Kushiriki katika mikutano ya Baraza au Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili pale inapoalikwa.
- Kulipa ada za Serikali na za Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa.

# Sehemu 14: Masuala ya Ujumla yanayogusa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

Asasi zote zenye dhima katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori zitazingatia yafuatayo:

## Uhusishwaji wa Masuala ya Kijinsia

Katika kuendesha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori maamuzi yote itabidi yazingatie jinsia, hali ya maumbile na umri wa watu.

Ili kutimiza lengo hili yafuatayo yatazingatiwa:

- Usimamiaji wa Rasilimali na maamuzi katika ngazi zote ndani ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yatoe kipaumbele mambo ya jinsia.
- Shughuli zote katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ziendane na sera husika pamoja na kanuni zihusuzo jinsia.
- Katika hatua za mwanzo, juhudi zielekezwe kwa wanawake katika Chama Wakilishi Cha Jumuiya ili kujenga uwezo wao kushiriki kikamilifu katika utawala na Hifadhi ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.
- Kamati zote zitakazoundwa na Chama Wakilishi Cha Jumuiya zisibague na zizingatie uwakilishi sawa na jinsia.
- Vifungu ndani ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999 vinavyohusu jinsia, viwe msingi wa utawala wa ardhi za vijiji zinazohusu Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori (Rejea: Vifungu vya 3, 20,23, 33, 35 na 45 vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji, 1999).

## Misaada kwa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

Kwa lengo la kufanikisha usimamiaji na uanzishwaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, utoaji wa misaada kama vifaa, fedha, huduma na utaalamu wa kiufundi kwa vijiji uzingatie Kanuni na Miongozo ifuatayo:

- Kila mtu anayetaka anaweza kutoa msaada kwa Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa.
- Idara ya Wanyamapori, Idara ya Uvuvi, Idara ya Misitu na Nyuki, Idara ya Utalii, TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Halmashauri za Wilaya zitalazimika kusaidia Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha malengo ya Sera ya Wanyamapori ya Tanzania, 1998.

- Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro zitasaidia katika Hifadhi ya Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori nje ya maeneo ya utawala wao, kulingana na Kanuni ya 33.

- Misaada itatolewa kwa lengo la kuyawezesha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori kujiendesha yenyewe.

- Katika kuhakikisha kwamba msaada unaotolewa unayawezesha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori kujitegemea, mashirika yatakayotoa msaada yatafanya yafuatayo:
  - Ainisha na kuorodhesha aina ya misaada.
  - Kuamua nyakati za kutoa msaada
  - Kuhusisha utoaji wa misaada na nyakati za kukoma kwake.

- Misaada yote itazingatia yafuatayo:
  - Uanzishwaji wa eneo
  - Uhamasishaji wa Jumuiya
  - Utekelezaji/Utawala
  - Uimarishwaji
    - Mwisho wa misaada
    - Kujenga uwezo (capacity buildling)

## Uinuaji wa Uwezo

Uinuaji wa uwezo utajumuisha upatikanaji wa elimu, mafunzo, na utoaji wa nyenzo bora za kuendeleza uwezo wa kiufundi na kitaalamu kwa wadau wote wa ngazi zote katika kuendeleza Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Ujenzi wa uwezo utazingatia yafuatayo:

- Kulenga vijiji, makundi/asasi (Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa, Halmashauri za Vijiji, Kamati ya maendeleo ya Kata, waajiriwa wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, Halmashauri za Wilaya (Wataalamu wa Maliasili; Baraza au Bodi ya Wilaya ya Ushauri) na wafanyakazi wa Chama Wakilishi Cha Jumuiya (watunza vitabu, viongozi wa kijiji nk).

- Mkurugenzi ataandaa mafunzo ya jumla au maalum kwa watu fulani au vikundi fulani vya wadau.

- Uwezeshaji utafanywa na mashirika ya wafadhili, NGO's, Idara ya Wanyamapori, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro au Hifadhi za Taifa, Wataalam wa Maliasili wa Wilaya, asasi za mafunzo ya wanyamapori na wataalamu wa sheria na utawala.

- Historia, muda na elimu ya walengwa, ujuzi wa kimila, jinsia, mahitaji yao, na uwezo wao wa kusimamia miradi yao.
- Mafunzo ya utunzaji wanyamapori yataongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori, 1998 na sera zingine zilizopo zinazohusu maliasili.
- Mkurugenzi atapitisha mitaala na muhtasari juu ya mafunzo ya utawala na Hifadhi ya wanyamapori.
- Chama Wakilishi cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kitaainisha mambo muhimu ya kujengewa uwezo na kutafuta nafasi au watu wa kuyaendeleza kwa kuwasiliana kwanza na Mkurugenzi.

## Uratibu wa Masuala yanayogusa Sekta Mbalimbali

Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili itakuwa na dhima ya kusawazisha au kuoanisha mambo ya sekta zingine ambayo yana mwingiliano wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja na Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Bodi au Baraza la Wilaya la Ushauri wa Masuala ya Maliasili katika ngazi ya wilaya au kati ya wilaya na wilaya itamshauri Mkurugenzi, Halmashauri za wilaya, Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa, Halmashauri za Kijiji /vijiji juu ya utekelezaji bora wa shughuli za Hifadhi yaMaeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori katika maeneo yaliyomo ndani ya himaya zao.

Bodi za Wilaya za Ushauri wa Masuala ya Maliasili zitaanzishwa kwa lengo la kuendeleza utaalamu na kutimiza matarajio ya kimaendeleo ya wilaya husika.

Kwa kushauriana na Bodi ya Wilaya ya Ushauri ya Maliasili, Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa kitawajibika kutambua sera za sekta, sheria, kanuni, miongozo, taratibu, mikataba na makubaliano ya kimataifa yanayohusu utawala na Hifadhi yaMaeneo ya Jumuiya ya Hifadhi yaWanyamapori. (Rejea: Kanuni ya 30).

# Utatuzi wa Migogoro na Usuluhishi katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori

*Ni nini kinaashiria kuwepo kwa Mgogoro?*

Inapotokea robo tatu ya wanachama wanataka kusitisha uanachama wao katika Chama Wakilishi cha Jumuiya itachukuliwa kuwa mgogoro umetokea na hivyo utapelekwa katika Kamati ya utaratibu wa usuluhishi, baraza au msuluhishi kama ambavyo itakuwa imeelekezwa katika katiba kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa katika mkataba wa Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori husika.

*Nini kifanyike mgogoro unapotokea?*

Endapo kutatokea mgongano wa maslahi, mawazo, au namna fulani juu ya uendelezaji wa Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori, ukijumuisha baadhi ya vijiji wanachama kujitoa katika Chama Wakilishi Cha Jumuiya, basi Kanuni zitaongoza juhudi zote za kuzuia au kusuluhisha mgogoro huo. (Rejea: Kanuni ya 30, 67, 68 na 69).

Inapotokea kuwa pande zinazohusika katika mgogoro ndani ya Eneo la Jumuiya la Hifadhi ya Wanyamapori, Katiba zao hazina kipengele juu ya utatuzi wa migogoro basi Sheria ya Usuluhishi itatumika.

Katiba ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya itatakiwa ieleze namna za kusuluhisha migogoro inapotokea.

Usuluhishi utaendeshwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Udhibiti na utatuzi wa migogoro, kwa kiwango kikubwa, utakuwa shirikishi, unaohimiza uwiano wa kijinsia, wazi na unaofuata Katiba na sheria za nchi.

*Haki na Wajibu wa Wadau*

Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili pamoja na mamlaka za wanyamapori zitahakikisha kwamba wadau wote wanajua haki na dhima zao katika kuendeleza Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori.

Baraza la Kijiji la Ardhi na Baraza la Kata zitasaidia kutatua migogoro inayotokea katika vijiji kulingana na vifungu vifuatavyo:

- Ibara za 60-63 vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999
- Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi ya 2002
- Sheria ya Mabaraza ya Kata ya 1985

Mgogoro baina ya Chama Wakilishi Cha Jumuiya Kilichoidhinishwa na mwekezaji utasikilizwa na Baraza la usuluhishi au Bodi ya Wilaya ya Ushauri wa Maliasili, ili kumaliza tofauti zao kwa amani nje ya mahakama.

## Makosa ya Jinai na Adhabu

Mtu yeyote anayekiuka au anayevunja kifungu chochote cha Kanuni hizi na kutiwa hatiani, atakuwa ametenda kosa.

Kanuni ya 70 na 71 ambazo hutoa makosa na adhabu, zitasimamiwa na mahakama zenye mamlaka kwa mujibu wa sheria zilizopo nchini.